

Kuongelea kuhusu VVU na mwenzi wako

Lineo anakitu kinacho msumbua akilini mwake ambacho anataka kumwambia mwenzi wake, lakini anaogopa kumpoteza. Angalia kuhusu uamuzi anaohitaji kuufanya kwakutazama katuni hapo juu. Ingekuwa ni wewe ungefanyaje?

Malizia hadithi ya Lineo kwa kutumia utunzi wa hadithi za michoro mtandaoni. Unaweza kushirikisha marafiki zako utunzi wako kwakutumia mtandao wowote wa kijamii unaoupenda.

[\[Katuni za michoro\]](#) [\[Karatasi ya ukweli\]](#) [\[Maelezo ya mwezesaji\]](#)

[>> WhatsApp Download <<](#)

Maelezo muhimu:

Kumwambia mwenzi wako kuhusu hali yako ya maambukizi ya virusi vya ukimwi inaweza ikawa ni vigumu na watu wengi wanahofia kukataliwa. Haya ni mambo machache ya kufikiria ili kijihisi tayari.

- Kumbuka kwamba huhitaji kuomba msamaha kwasababu tu unaishi na virusi vya ukimwi.
- Kabla ya kuongea na mwenzi wako itasaidia zaidi ukiwa na taarifa kamili zitakazo fanya aelewe zaidi pale utakapo mwongelea. Anaweza dhani kwamba ukiwa na virusi vya ukimwi utakuwa unamaanisha kuwa huna maisha marefu mbeleni, au hutakuwa na uwezo wa kufanya ngono salama mbeleni au hata kuwa na familia. Kama utaweza kumsaidia kuelewa ukweli kuhusu virusi vya ukimwi na kumhakikishia kuwa ana uwezekano mdogo wa kulipokea hili vabaya.
- Fikiria kuhusu wakati sahihi wa kuzungumza nao - wakati ambao hawana haraka ya kwenda mahali fulani au wakati ambao hawana msongo wa mawazo.
- Tafuta mahali ambapo hamtasumbuliwa ili uwe na muda wa kutosha kumueleweshwa. wape muda wa kuelewa kile unachokisema. Hakikisha kama ameelewa pia uwa ruhusu kuuliza maswali.
- Mwitikio wowote mwenzi wako atakaonyesha mwanzoni, fahamu yakuwa unaweza kubadilika kadri muda utakavyoongrdeka.
- Kama hamkufanya ngono salama na mwenzi wako, nimuhimu kwenda kupima. Mara tu baada ya kufahamu hali zenu mnaweza kuamua kutumua njia sahihi Zaidi za kufanya ngono salama.
- Hofu na unyanyapaa vinaweza kuchochea hisia kali sana. Kuwa tayari kwamba hali yako inaweza kuwafanya watu wengine wakuogope au wakuhukumu. Kumbuka kuwa wewe bado ni wewe na hali yako haikutambulishi.
- Na kumbuka... Kuzungumza na rafiki au mtu wa familia ambaye unayemuamini kuhusu hali yako ya virusi vya ukimwi inaweza kukusaidia mchakato wa mawazo yako na hisia zako. Haupaswi kamwe kuhisi unashurutishwa kusema hali yako kwa mtu yeyote ambaye haumwamini. Ikiwa hivi karibuni umegundua unavirusi vya ukimwi Usiwahi hisi ulazima

wa kumwambia yeyote. Ikiwa ndiyokwanza umefahamu kuwa umeambukizwa virusi vya ukimwi, itakuwa ni busara kujipatia muda ili kuizowea hali na uweze kujiandaa vizuri kuwaeleza wengine.

Mawazo ya mjadala:

- Unafikiri kuna faida gani kwako na mwenza wako kuweka wazi kuhusu hali yangu? Fikiria angalau faida tatu kwa kila mmoja wenu.
- Kwanini unafikiri inaweza kuwa ni vigumu na inaamsha hisia kumwambia mtu ambaye ni mwenzi wako wa sasa au wa zamani juu ya hali yako ya virusi vya ukimwi?
- Ikiwa uko kwenye mahusiano, fikiria mwenzi wako angekuwa na mwitikio gani kama ungemwambia una virusi vya ukimwi. Je! Ungekuwa na mwitikio gani kama wangekuambia walikuwa virusi vya ukimwi?
- Nje! ni mahali gani (au watu gani) katika jamii yako au karibu yako, unafikiri wanaweza kukupa msaada, au kukusaidia kufikiria kuhusu mwitikio unaoweza kutokea.
- Unadhani kumwambia mwenzi wako kunaweza kubadilisha uhusiano wako na hisia zako kwa kila mmoja? Fikiria njia zote mbili ambazo zinaweza kuharibu na kuboresha uhusiano wako.
- Ikiwa unaishi katika jamii ndogo au eneo la kijiji unafikiri ni mambo gani ambayo unahitaji kufikiria na kujiandaa wakati wa kumwambia mwenzi?
- Unadhani ni maswali gani ambayo mwenza wako atakuwa nayo kwanza?
- Unahaki ya kulinda faragha yako mwenyewe, na mwenzi wako anahaki ya kutarajia ukweli kutoka kwako. Je! Ni ipi muhimu Zaidi, faragha au ukweli?
- Kama mwenza wako au rafiki akikwambia ukweli kuhusu hali yake, je utalipokeaje? Au utawasaidiaje?

Young Voices Africa ni kikundi kinacho jadili kuhusu mijadala mbalimbali ya afya ya uzazi na kufanya ngono salama. Kimekuwa kikiendelezwa na vijana na nikwaajili ya vijana kuanzi miaka 15 mpaka 24 nchini Afrika ya kusini.

Last full review:

10 March 2021

Next full review:

10 March 2022